

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3
Baruapepe: cg@dcea.go.tz
Tovuti: www.dcea.go.tz
Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni
S.L.P. 80327
Dar es Salaam
Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

WATATU WAKAMATWA NA DAWA ZA KULEVYA AINA YA HEROIN.

Dar es Salaam, 27 Januari 2021:

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inawashikilia watuhumiwa watatu kwa tuhuma za kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya aina ya Heroin. Watuhumiwa hao ni **ANADHATI RASHID MCHONGEZA** umri miaka 20, **EMMANUEL MSAKUZI** umri miaka 23, na **KULWA PAZI SHAMAS** umri miaka 49, almarufu mama udodi ambaye pia ni balozi wa nyumba 50 katika mtaa wa JUWAJE Kunduchi Pwani.

Watuhumiwa walikamatwa tarehe 22 Januari, 2021 katika eneo la Kunduchi Pwani Kauzeni Jijini Dar es salaam, wakiwa na unga unaodhaniwa kuwa ni dawa za kulevya aina ya Heroin kiasi cha gram 400 na majani makavu ya bangi puli moja (**kiasi hicho ni sawa na kete 30 za bangi**).

Maafisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya baada ya kufanya upekuzi walifanikiwa kukamata kiasi cha dawa hizo zikiwa zimehifadhiwa ndani ya mfuko wa nailoni. Mamlaka inaendelea kuwashikilia watumumiwa na watafikishwa mahakamani baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Kadhalika, katika kipindi cha mwezi Novemba mpaka Disemba 2020, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ilifanikiwa kushinda kesi kubwa tatu zilizowahusisha mapapa wa biashara ya dawa za kulevya ambazo ni;-

Mosi, mfanyabiashara maarufu jijini Tanga **Yanga Omari Yanga** maarufu kama **Raisi wa Tanga** na kuhukumikiwa kifungo cha miaka 30 jela baada ya kukutwa na hatia ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kiasi cha gramu 1052.63.

Pili, Mahakama Kuu ilimkuta na hatia Ayubu Mfaume Kiboko na Mkeke Pili Kiboko na kuwahukumu kifungo cha miaka 20 gerehani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin zenye uzito wa gramu 251.25.

Tatu, raia wawili wa Iran walitiwa hatiani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin yenye uzito wa kilogramu 111.02 katika Bahari ya Hindi na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela pamoja na kutaifishwa kwa jahazi husika.

Pia katika kipindi hicho, Mamlaka imefanya operesheni mbalimbali na kufanikiwa kumkamata Kibinda Mohamed Selemani akiwa na dawa za kulevya aina ya heroin kiasi cha gramu 135.12. Mtuhumiwa ameshafikishwa mahakamani.

Mwaka 2020, Mamlaka imefanikiwa kufungua vituo vingine vitatu vya kutolea tiba ya methadone Tanga, Bagamoyo na hospitali ya Tumbi Pwani.

Pamoja na vituo hivyo vipya, Mamlaka imeongeza wigo wa upatikanaji wa tiba ya uraibu wa dawa za kulevya kwa kuongeza vituo vingine vitatu vya kutolea tiba ya methadone “satellite clinics” jijini Dar es Salaam maeneo ya Segerea, Mbagala rangi tatu na Tegeta vinavyotarajia kuanza kutoa huduma hiyo mwezi ujao Februari, 2021. Hiyo inafanya Jiji la Dar es Salaam kuwa na jumla ya vituo sita (6) kati ya tisa (9) vinavyotoa tiba ya methadone nchini ili kupunguza msongamano uliokuwa katika vituo vitatu vya awali.

Aidha, Mamlaka inatarajia kuzindua kituo cha tiba ya methadone mkoani Arusha hapo tarehe 15 Februari, 2021 kitakachohudumia kanda ya Kaskazini. Mikoa mingine iliyokuwa na vituo vya tiba ya methadone ni Mbeya, Mwanza na Dodoma. Hadi sasa vituo hivi vimeweza kutoa huduma kwa waraibu 9,500 nchini.

Huduma ya upataji nafuu inaendelea katika nyumba 25 “sober houses” zilizopo maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia mwezi Desemba 2020 kulikuwa na waraibu wapatao 3,663 walionufaika na huduma hiyo, kati yao 3,609 wakiwa wanaume na 74 wanawake.

Elimu

Mamlaka inaendelea kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa njia mbalimbali ikiwemo matukio makubwa ya kitaifa na vyombo vya habari. Aidha, Mamlaka imeandaa Mwongozo wa

Uelimishaji kwa Wadau wanaofanya uelimishaji kwa makundi mbalimbali ya kijamii unaotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa fedha.

Aidha, katika kudhibiti na kuzuia uchepushwaji wa kemikali bashirifu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya, Mamlaka kwa kushirikiana na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali tumetoa mafunzo kwa wadau mbalimbali zaidi ya 500 wakiwemo madereva wa malori, wasimamizi wa shughuli zinazohusu kemikali, wajasiriamali wanaotumia kemikali pamoja na maafisa biashara, na maafisa wa serikali wanaohusika kudhibiti wa kemikali hizo

Tunaendelea kuwakumbusha Watanzania wote kutambua tatizo la dawa za kulevya kuwa ni mtambuka hivyo tunahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali pamoja na Jamii kwa ujumla. Hivyo basi naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba Umma kwa ujumla wake kushiriki kwa dhati kabisa katika kukabiliana na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini, Hasa kuwafichu wanaojihusisha na biashara hii haramu.

Imetolewa na,

Lilian Matho



Afisa Mawasiliano

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.